## 1.0. JINA NA IMANI

1.1. Jina la Chama litakuwa Chama cha Wafanyakazi Mashambani na Kilimo Tanzania. “TANZANIA PLANTATION AND AGRICULTURAL WORKERS UNION” kwa kifupi TPAWU.

1.2. **Makao Makuu ya Chama:**

Makao Makuu ya Chama yatakuwa Dar es Salaam na anuani yake itakuwa S.L.P.77420, DAR ES SALAAM.

1.3. **Kujishirikisha hapa Nchini**:

Chama kitajishirikisha na ***Shirikisho la Vyama vya Wafanyakazi Tanzania (TUCTA)*** na kitawawakilisha wanachama wote wanaotokana na sehemu za kazi za mashambani na kilimo na wale ambao kwa uamuzi wa TUCTA watakuwa wanachama wa Chama hiki ***ikiwa ni pamoja na sekta isiyo rasmi***.

1.4. **Ushirikiano na nje:**

Chama hiki kitakuwa na uhusiano wa karibu na vyama vingine vya Sekta ya Kilimo katika nchi mbalimbali na kujiunga ***Interational Union of Food (IUF).***

1.5. **Imani ya Chama**

Chama kinaamini kuwa:

(a) Wafanyakazi wote duniani ni sawa.

(b) Kila mfanyakazi ana haki ya kufanya kazi na anastahili malipo kufutana na kazi hiyo pamoja na kuheshimiwa kama binadamu.

(c) Mshikamano wa wafanyakazi wote duniani ndiyo njia pekee itakayokuza ushirikiano wa karibu kati ya wafanyakazi na vyama vyao katika nchi zote.

(d) Nguvu ya wafanyakazi itatokana na juhudi zao katika kukuza umoja.

(e) Utengano wa aina yoyote kati ya wafanyakazi ni udhaifu.

(f) Kila mfanyakazi atakuwa huru kujiunga na Chama chochote cha siasa atakachopendelea.

(g) TPAWU ni Chama ambacho hakitajishirikisha rasmi na Chama chochote cha siasa nchini.

**2.0. MADHUMUNI:**

2.1.Madhumuni Makuu ya Chama yatakuwa yafuatayo:

2.1.1. Kuwaunganisha wafanyakazi, kulinda, kutetea na kuendeleza haki na maslahi yao wawapo kazini na wanapostaafu.

2.1.2. Kushirikiana na kujadiluiana na waajiri katika kudumisha amani mahali pa kazi

2.1.3. Kujadiliana na kuondoa ukandamizaji na ubaguzi wowote baina ya mwajiri na mfanyakazi.

2.1.4. Kutekeleza na kusaidia katika utekelezaji wa mikataba ya Hali Bora za kazi na Tuzo. Kanuni za nidhamu na kanuni zozote zile ambazo zinatumika nchini.

2.1.5. Kushirikiana na kubadilishana ujuzi na vyama vingine vya wafanyakazi nchini pamoja na vile vya Kimataifa kwa madhumuni ya:

(a) Kupata, kutunza na kutoa taarifa au elimu katika masuala muhimu yahusuyo vyama vya wafanyakazi.

(b) Kubadilishana ujuzi au taarifa katika masuala yanayohusiana na mishahara na hali za wafanyakazi na taratibu za Kimataifa zinazohusiana na masuala hayo.

2.1.6. Kuwasiliana na Serikali kuhusu haja ya kutunga sheria sahihi za kazi na kuandaa sera nzuri za kuendeleza uchumi na maisha ya jamii.

2.1.7. Kulinda maslahi ya wanachama kwa kuisaidia Serikali kuepukana na uandaaji wa sera ambazo ni hatari kwao.

2.1.8. TPAWU itakuwepo kwa ajili ya kutoa huduma kwa wanachama na si kwa kujipatia faida.

## 3.0. UANACHAMA:

3.1. Maombi ya Uanachama

3.1.1. ***Wafayakazi wote waliokuwa OTTU na kujiunga na TPAWU baada ya kuanzishwa kwake ndiyo walikuwa waanzilishi wa chama***.

3.1.2. Mwanachama wa TPAWU sharti awe mfanyakazi wa sekta zilizoainishwa katika Katiba hii.

3.1.2.1. Sekta na sehemu za kazi:

Uanachama utagawanyika katika sehemu na sekta kufuatana na aina ya kazi za wanachama kama ifuatavyo:

(a) Wafanyakazi katika mashamba ya miwa, makampuni ya sukari na viwanda yake.

(b) Wafanyakazi katika mashamba ya katani/mkonge na viwanda vinavyotengeneza bidhaa zitokanazo na zao la mkonge.

(c) Wafanyakazi katika mashamba ya chai na viwanda vyake.

(d) Wafanyakazi walioajiriwa katika mashamba ya korosho, misitu, nafaka, mifugo, tumbaku, Pareto, pamba, kahawa, mashamba mchanganyiko na mazao na viwanda vyake.

(e) Wafanyakazi katika vyama vya ushirika, makampuni ya mazao, makampuni ya ununuzi wa mazao ya kilimo, mamlaka ya mazao na viwanda vyake na watendaji katika chama.

(f) Wafanyakazi katika mashamba ya Maua, mbogamboga, matunda, migomba, mazao mengine ya kilimo na viwanda vyake.

(g) ***Wafanyakazi katika sekta isiyo rasmi.***

3.1.3. Maombi ya wanachama yatapelekwa kwenye Halmashauri ya tawi mahali pa kazi anapofanyia kazi mwombaji. Pale ambapo hapana Tawi maombi yatapelekwa katika ofisi ya chama iliyo karibu.

3.1.4. Halmashauri ya Tawi bila kuchelewa itayafikiria maombi. Kamati ya tawi itakayokataa maombi, itawajibika kutoa sababu za uamuzi huo kwa mwombaji.

3.1.5. Uamuzi wa kamati ya tawi utanzia siku maombi yalipopokelewa na mwanachama atapewa kadi ya uanachama.

**3.2. Michango ya mwanachama**

3.2.1. Baada ya maombi ya uanachama kukubaliwa atalipa kiingilio kwa kiwango ambacho kitaamriwa na Baraza Kuu la Chama na atapewa stakabadhi. Baada ya kulipa kiingilio wanachama wapya watapewa kadi za uanachama.

**3.2.2. Michango ya kila mwezi:**

3.2.2.1. Wanachama watalipa michango yao kila mwezi katika kiwango cha asilimia 2 ya mshahara wa mwanachama na kiwango kinaweza kikabadilika kufuatana na uamuzi wa Mkutano Mkuu wa Chama.

3.2.2.2. Michango ya kila mwezi italipwa kwa utaratibu ufutao:

(a) Mwanachama anaweza akapeleka michango yake moja kwa moja ofisi ya chama na akapewa stakabadhi.

(b) Michango ya wanachama itapelekwa kwenye chama na mwajiri.

(c) Malipo yote yatakayofanywa na wanachama yatapelekwa Benki katika akaunti iliyofunguliwa na chama.

**3.2.3. Ada maalum:**

Kila watakapotakiwa, wanachama watawajibika kutoa ada maalum kwa kadri itakavyoamuliwa na Kamati ya Utendaji ya Taifa katika masuala yanayohusiana na migomo, maendeleo ya Chama au matatizo mengineyo mahali pa kazi.

**MATUMIZI YA FEDHA ZA CHAMA:**

Fedha za Chama zitatumika kwa madhununi ya kugharamia shughuli mbalimbali za Chama kama itakavyoamuliwa na vikao vya Chama na Katibu Mkuu.

**3.3. Uanachama wa Heshima:**

3.3.1. Uanachama wa heshima unaweza kutunukiwa kwa wanachama waasisi waliojitolea wakati wa enzi wao katika kukiendeleza Chama.

3.3.2. Uchaguzi (uteuzi) wa uanachama wa heshima utafanywa na Mkutano Mkuu wa Chama.

3.3.3. Wanachama wa heshima hawataruhusiwa kupiga kura katika Mikutano ya Chama.

**3.4. Mchango wa huduma za Chama kwa wafanyakazi wasiokuwa wanachama:**

3.4.1 Mahali popote pa kazi ambapo wanachama watazidi 50% (asilimia hamsini) ya wafanyakazi wote walioajiriwa, mwajiri atalazimika kuchangisha fedha kwa ajili ya Chama kutoka katika mishahara ya wafanyakazi wasiokuwa wanachama na kupeleka fedha hizo katika ofisi au akaunti ya Benki ya Chama. Kiwango cha mchango kitakuwa sawa na mchango wanayotoa wanachama.

**3.5. Kadi za Uanachama na uandikishaji**

3.5.1. **Kadi za uanachama:**

Kila mwanachama atapewa kadi iliyochapishwa ambayo ndani yake itajaza jina lake, anuani yake, kazi yake, nambari yake, tarehe ya ujiunga na Chama, jina la Chama na maelezo mengine yoyote kama itakavyoelekezwa na kanuni au taratibu za Chama.

**3.5.2. Daftari la Kumbumbuku:**

Baada ya kukubaliwa kujiunga na Chama, maelezo yote ya mwanachama huyo yaliyomo katika kadi ya uanachama yataingizwa katika daftari la kumbukumbu za Chama kwa madhumuni ya kusaidia kuweka kumbukumbu za michango ya wanachama, na kumbukumbu hizo zitatakiwa kuwa sahihi kila wakati.

**3.6. Haki za Mwanachama:**

3.6.1. Mwanachama yeyote, mbali na wanachama wa heshima atakuwa na haki zifuatazo:

(a) Kuwakilishwa na chama dhidi ya mwajiri wake pamoja na haki ya yeye mweyewe kujitetea dhidi ya mwajiri huyo kwa mashtaka yoyote dhidi yake.

(b) Kujitetea mbele ya vyombo mbalimbali vya chama na haki ya ***kukata*** rufaa katika vikao vya juu vya chama kama hataridhika na uamuzi uliotolewa.

(c) Kushiriki katika uchaguzi wa uongozi wa chama kwa mujibu wa kanuni zilizopo.

(d) Kushiriki katika shughuli zote za chama na mikutano kwa mujibu wa kanuni zilizopo.

(e) Kuwa na haki ya kuweza kufahamu mali za chama.

**3.7. Wajibu wa Mwanachama:**

3.7.1. Kila mwanachama atakuwa na wajibu wa:-

(a) Kulipa michango ya kila mwezi na mchango maalum kwa wakati unaotakiwa.

(b) Kuunga mkono na kusaidia kwa vitendo maendeleo ya chama.

(c) Kuzingatia katiba na taratibu za chama na kuheshimu maamuzi yaliyotokana na katiba au taratibu hizo.

(d) Kuhudhuria vikao vyote vya chama vinavyomhusu.

(e) Kuheshimu uamuzi uliokubaliwa na wengi

(f) Kuhakikisha kuwa anatekeleza kanuni za kazi na anatumia ujuzi, elimu na uwezo ili kuinua ufanisi katika kazi.

**3.8. Kuacha uanachama:**

3.8.1. Mwanachama ambaye hatalipa michango yake kwa miezi sita mfululizo bila sababu za msingi zinazokubaliwa na Halmashauri ya tawi/ofisi ya Katibu Mkuu atakuwa amejiachisha uanachama.

**3.8.2. Kujiuzulu Uanachama:-**

3.8.3. Mwanachama anaweza kutoa notisi ya ***siku 30*** kujiuzulu uanachama wake kwa kuandikia Halmashauri ya tawi lake. Tawi litapaswa kumtaarifu Katibu wa ***Sehemu***/Kanda.

3.8.4. Mtu yeyote ambaye uanachama wake utakwisha katika chama hatakuwa na haki wala kuhusika na mali ya chama.

**3.9. Kufukuzwa Uanachama:**

3.9.1. Mwanachama yeyote au Afisa wa kuchaguliwa au wa kuteluliwa anaweza kufukuzwa uanachama kama:

(a) Atagundulika kuwa alijipatia uanachama kwa njia ya udanganyifu.
(b) Kwa kukosa uaminifu au amefuja mali ya chama.
(c) Amegundulika kuwa ni mwanachama wa chama kingine kinachoshindana na chama hiki.
(d) Atafanya vitendo vinavyopingana na kanuni za chama au uamuzi wa Mkutano Mkuu wa chama.
(e) Amekosa uzalendo na utii kwa chama kwa mfano kuhusiana na masuala ya kukisaliti chama katika migogoro ya kikazi.

3.9.2. Utaratibu wa kumfukuza mwanachama katika chama:

(a) Endapo mwanachama ataonekana ana dosari atapewa nafasi ya kujitetea kabla ya hatua nyingine hazijachukuliwa.

(b) Halmashauri ya tawi itatoa taarifa za shauri hilo kwa Kamati ya Utendaji ya Kanda ya chama pamoja na mapendekezo ya kumfukuza mwanachama.

(c) Kamati ya Utendaji ya Kanda itapeleka taarifa ya uamuzi wake kwa mwanachama aliyependekezwa kufukuzwa uanachama kwa maandishi.

(d) Mwanachama aliyefukuzwa uanachama na Kamati ya Utendaji ya Kanda atakuwa na haki ya kuomba rufaa dhidi ya uamuzi huo kwa Kamati Kuu ya Utendaji Taifa ambayo itakuwa na uamuzi wa mwisho.

**3.10. Kuhama Uanachama:**

3.10.1. Mwanachama ambaye ajira yake itakwisha mahali pake pa kazi atatoa taarifa kwa Halmashauri ya Tawi lake ambalo litatia muhuri kwenye kadi yake kuthibitisha kuwa alitimiza masharti yaliyomo katika katiba ya chama.

3.10.2. Kuhama kwa mwanachama kutoka sehemu moja ya kazi kwenda sehemu nyingine katika chama Mwanachama anayehama sehemu moja ya kazi kwenda sehemu nyingine katika chama hiki atatoa taarifa katika Tawi la karibu la mahali pengine pa kazi au sehemu na kuendelea kuwa mwanachama wa chama hiki.

**4.0. MATAWI YA CHAMA:**

4.1. Chama kuanzishwa matawi.

4.1.1. Kamati ya Utendaji ya Kanda itaanzisha matawi katika kila mahali pa kazi ambapo wanachama kumi au zaidi wameajriwa.

4.1.2. Wanachama walioajiriwa mahali pa kazi ambao hawafiki watu kumi watahudumiwa na mwakilishi mmoja wa chama atakayechaguliwa miongoni mwao kuwakilisha maslahi yao kwa niaba ya chana (Shop Steward)

4.1.3. Kila Tawi litaandikishwa Makao Makuu ya chama.

4**.2. Vikao vya Tawi:**

4.2.1. Vikao vya Tawi vitakuwa kama ifuatavyo:
(a) Halmashauri ya tawi.
(b) Mkutano wa wanachama wote.
(c) Mkutano wa wafanyakazi wote.

4.2.2. Mikutano yote ya wafanyakazi iliyotajwa hapo juu itafanyika kama ifuatavyo:
(a) Mkutano wa Halmashauri ya Tawi utafanyika mara moja kwa mwezi
(b) Mkutano wa wanachama wote utafanyika mara mbili kwa mwaka.
(c) Mkutano wa wafanyakazi wote utafanyika mara moja kwa mwaka.

**4.3. Muundo wa Vikao vya Chama.**

4.3.1. Halmashauri ya Tawi itakuwa na wajumbe wafuatao:-

***(a) Mjumbe 1 kwa wanachama 1 – 9.***
***(b) Wajumbe 3 kwa wanachama 10 – 20.***
***(c) Wajumbe 10 kwa wanachama 21 – 100.***
***(d) Wajumbe 15 kwa wanachama 101 na kuendelea***
***(e) wajumbe waliotajwa katika a – d hapo juu watajumuisha Mwenyekiti wa Kamati ya Wanawake na Mwenyekiti Kamati ya Vijana.***
(f) Idadi ya uwakilishi inaweza kubadilika kufuatana na matakwa ya sheria za kazi.

**4.3.2. KAZI ZA HALMASHAURI YA TAWI:**

Halmashauri ya tawi itafanya kazi zifuatazo:
(a) Kulinda, kutetea na kuendeleza haki na maslahi ya wanachama wake na kuhakikisha kuwa afya na usalama vinadumishwa mahali pa kazi.

(b) Kuandaa na jkuwasilisha mikataba ya hali bora za kazi kwa Katibu wa Kanda na Katibu Mkuu ili iweze kupitiwa na Makao Makuu kwa majadiliano na mwajiri.

(c) Kubuni njia za kukuza tija na kuendeleza uzalishaji na ajira ya hakika na kuhakikisha kuwa wanachama wanafaidika kutokana na ziada inayotokjana na ongezeko la tija.

(d) Kutoa taarifa mara kwa mara kwa wanachama kuhusu shughuliza ujumla za tawi.

(e) Kuingiza wanachama wapya

(f) Kuhakikisha kuwa kifungu cha 3 kinachohusiana na uanachama na michango (3.2.2.) kufukuzwa uanachama (3.9) na kuhama uanachama (3.10) vinatekelezwa.

(g) Kuendeleza uhusiano kati ya wafanyakazi na mwajiri na kati ya matawi mengine yenye kazi za aina moja.

(h) Kuendeleza na kusimamia elimu ya wafanyakazi

(i) Kutoa misaada na ushauri kwa wanachama.

(j) Kupanga na kushughulikia fedha za chama.

(k) Kutunza vitabu vya kumbukumbu za chama

(l) Kutoa taarifa ya mapato na matumizi kwa wanachama

(m) Kuhakikisha kuwa Kamati za Afya na Usalama na Kamati za wanawake zina anzishwa na kuimarishwa mahali pa kazi.

(n) Kutoa onyo au kumsimisha uongozi wakati pendekezo la uongozi litakapopelekwa kwa Kamati ya utendaji ya Kanda kwa uamuzi wa mwisho, pale kiongozi atakapobainika hafuati masharti ya katiba au kutokuwa na nidhamu.

### 4.4. Halmashauri ya Tawi:

4.4.1. Halmashauri ya tawi itaitisha mikutano yake angalu mara moja kila mwezi mmoja ingawa kunaweza kjuitishwa kikao cha dharura kwa uamuzi wa Katibu wa Tawi baada ya kushauriana na Mwenyekiti wake.

4.4.2. Mwenyekiti wa Tawi atakuwa kiongozi wa mikutano yote ya Halmashauri ya tawi. Endapo Mwenyekiti wa tawi atakuwa na udhuru wa kumfanya asihudhurie mkutano, wajumbe watachagua miongoni mwao Mwenyekiti wa muda.

4.4.3. Endapo kunatokea mgogoro wa kikazi mahali pa kazi, kamati ya tawi itaitisha mkutano wa wanachama wote na kama ni mahali ambapo muafaka umeshindikana na mwajir, kura ya maoni ya kuhusu uwezejkano wa kuitisha mgomo itapigwa.

4.4.4. Uamuzi wa kutangaza mgomo utahitaji theluthi mbili ya wanachama, Halmashauri ya tawi itawasilisha mapendekezo ya mgomo kwa Katibu wa sehemu/kanda yakitaja tarehe ya mgomo.

4.5. **Mkutano wa Wanachama wote**:

4.5.1. Mkutano wa wanachama wote utafanyika kila baada ya miezi sita au wakati wowote inapotokea dharura.

**Mkutano wa wanachama wote utakuwa na kazi zifuatazo:**

(a) Kupokea na kujadili taarifa ya Halmashauri ya tawi na kuagiza Halmashauri hiyo katika utekelezaji wa mambo yatokanayo na taarifa hiyo.

(b) Kupokea na kujadili njia za kutekeleza maamuzi yaliyopitishwa na vyombo vya Sehemu, Kanda, Taifa na mambo yoyote tayatakayoletwa na wanachama katika tawi.

(b) Kuchagua viongozi

(i) Mwenyekiti wa Tawi

(ii) Katibu wa Tawi

(iii) Halmashauri ya Tawi

(iv) Wawakilishi katika Mkutano Mkuu wa Kanda

(v) Kupokea taarifa ya mapato na matumizi ya chama tawini kutokana na asilimia kumi (10%) ya mapato ya ada za wanachama yanayoachwa au mradi wa chama uliopo tawini.

(d) Kupitisha makisio ya mapato na matumizi ya chama tawini kwa mwak unaofuata.

4.5.2. Mkutano wa wafanyakazi wote katika tawi utafanyika mara moja kwa mwaka na utafanya yafuatayo:

(a) Kujadili utekelezaji mzuri wa mpango wa kazi kama ulivyowasilishwa na Halmashauri tawi.

(b) Kujadili taarifa ya utendaji iliyowasilishwa na kutano wa Baraza la wafanyakazi

**4.6. Uchaguzi wa tawi**

4.6.1. Ni wanachama hai tu ndio watakaoruhusiwa katika kikao cha wanachama wote.

4.6.2. ***Ni wanachama hai tu ndiyo watakuwa na haki ya kupiga na kupigiwa kura kwa nafasi za uongozi ngazi ya Tawi, Kanda na Taifa***.

**4.7. Kamati ya Usimamizi ya Uchaguzi:**

4.7.1. Kutakuwepo na kamati ya usimamizi itakayoundwa na wajumbe watatu ambao ***watachaguliwa na mkutano wa tawi kabla ya mkutano mkuu wa uchaguzi kuanza au maafisa wa chama***.

4.7.2. Mapendekezo yote ya wagombea yatawasilishwa katika kamati ya usimamizi ya uchaguzi wiki tatu kabla ya mkutano wa wanachama katika tawi ambao ndio wa uchaguzi.

**4.7.3. Kazi za Kamati ya Usimamizi ya uchaguzi ni hizi zifuatazo:**

(a) Kuhakikisha kuwa kuna mapendekezo ya kutosha kwa nafasi zote za wagombea.

(b) Kuhakikisha kwamba ni wanachama wasilaza michango yao ya kila mwezi ndio walioruhusiwa kuingia katika kikao cha mkutano wa mwaka wa wanachama wote.

(c) Kuwasilisha katika kikao orodha yote ya mapendekezo pamoja na taarifa inayoelezea kuwa ni nani kati ya waliopendekezwa hawafai kugombea uongozi kwa mujibu wa katiba ya chama.

(d) Kamati ya usimamizi ya uchaguzi itasimamia uchaguzi ikiwa ni pamoja na kutaja idadi sahihi ya wajumbe wenye haki ya kupiga kura.

4.7.4. Taarifa na mapendekezo ya Kamati ya utendaji ya uchaguzi itawasilishwa katika kikao ili kiweze kupitia na kuikubali.

4.7.5. Uchaguzi utafanyika katika mkutano wa mwaka wa wanachama wote. Hata hivyo mkutano maalum unaweza kuitishwa kwa ajili ya kujaza nafasi iliyoachwa wazi ya Mwenyekiti au Katibu wa tawi aliyejiuzulu au kulazimika kuacha kiti kwa sababu zozote zile kabla ya muda wa uchaguzi wa kawaida.

4.7.6. Wajumbe wa Halmashauri ya tawi pamoja na Mwenyekiti na Katibu wa Tawi watachaguliwa kila baada ya mika mitano(5).

4.8. Uchaguzi wa wawakilishi katika Mkutano Mkuu wa Kanda.

4.8.1. Kila tawi litakuwa na wawakilishi ***wanne (4)*** katika Mkutano Mkuu wa Kanda: Mwenyekiti, Katibu, Mwenyekiti wa Kamati ya **Wanawake *na Mwenyeviti wa Kamati ya Vijana.***

4.8.2 ***Wagombea binafsi ambao ni wanachama hai na siyo wajumbe wa mkutano mkuu wa Kanda au Taifa, wataruhusiwa kugombea nafasi ya uongozi katika ngazi ya Kanda au Taifa. Gharama za mgombea binafsi zitabebwa na mgombea mwenyewe.***

**4.9. Viongozi wa tawi na kazi zao:**

4.9.1. Mwenyekiti wa Tawi:

4.9.2. Mwenyekiti wa tawi atafanya kazi zifuatazo:

(a) Ataongoza mikutano yote ya tawi kwa uangalifu na utulivu.
(b) Atatia sahihi katika Kumbukumbu za mikutano pamoja na Katibu wa Tawi.
(c) Atasimamia utendaji wa kazi katika tawi ikiwa ni pamoja na kuhamasisha wafanyakazi kuingiza wanachama wapya
(d) Kusimamia mapato na matumizi ya fedha za chama katika tawi.

4.9.3. Endapo Mwenyekiti kwa sababu yoyote ile hataweza kuhudhuria Mkutano, Halmashauri ya tawi itachagua mjumbe mmoja wapo kusimamia mkutano huo

4.9.4. Katibu wa Tawi:

4.9.5. Katibu wa Tawi atafanya kazi zifuatazo:-

(a) Atatunza vitabu vya hesabu za fedha na hati za tawi na kuendeleza vipindi vya mwaka wa fedha katika kitabu cha michango na katika masalio ya kazi za mwanachama.

(b) Atahudhuria mikutano yote ya tawi na kutia sahihi na kutunza kumbukumbu za mijutano hiyo.

(c) Atafanya mawasiliano yote yanayohusika katika tawi na kuwasomea wanachama iwapo kutakuwa na haja hiyo.

(d) Atawasilisha kwa Katibu wa ***Sehemu/***Kanda taarifa ya wanachama wote katika tawi pamoja na tarehe waliyojiunga na chama nambari za kadi wao na masalio ya malipo kwa wanachama husika.

(e) Atawasilisha taarifa ya fedha zote alizopokea kwa niaba ya tawi kwa Katibu ***wa Sehemu/***Kanda kila mwezi baada ya kuondoa fedha ambazo ameruhusiwa kubakisha kwa matumizi ya tawi.

(f) Atawasilisha katika Halmashauri ya tawi kila miezi mitatu taarifa ya mapato na matumizi ya fedha za chama pamoja na taarifa ya idadi ya wanachama maendeleo ya chama kwa ujumla.

(g) Atatengenezaq mizania ya kila mwezi itakayoonyesha kwa usahihi mapato na matumizi ya tawi. Kama kuna matatizo yatakayojitokeza kuhusiana na michango na taarifa basi Katibu wa Kanda apewe taarifa.

(h) Kila itakapobidi ataitisha mikutano maalumu ya tawi baada ya kushauriana na Mwenyekiti.

(i) Kama atajiuzulu yeye mwenyewe, au ataacha ukatibu kwa ajili ya umri, au atalazimishwa kuacha, atakabidhi kwa Mwenyekiti wa tawi vitabu na mali za chama au mauzo ya mali hizo kwa mujibu wa katikba ya chama kamati ya tawi itamteua Katibu wa muda na kumkabidhi shughuli zote za chama mpaka uchaguzi utakapofanyika.

5.0. **Muundo wa Kamati za Wanawake**:

5.1. Zitaanzishwa Kamati za Wanawake sehemu za kazi kuanzia ngazi za matawi, Kanda na Taifa ambazo zitafanya kazi zake chini ya chama matawini, Kanda na Taifa.

Kamati ya wanawake wafanyakazi ngazi ya tawi itakutana kabla ya Halmashauri ya Tawi.

5.2. **MUUNDO WA KAMATI**

Kamati ya tawi sehemu ya kazxi yenye wafanyakazi wanawake
1 – 5- Wajumbe wane (4)
51- 100 – wajumbe watano (5)
101 – Kuendelea wajumbe sita (6)

**5.3. Kamati ya Wanawake Kanda**

5.3.1. Kamati ya utendaji ya wanawake Kanda itakuwa na wajumbe wasiopungua watano Wenye sifa zifuatazo:
(i) Watokane na Mkutano Mkuu wa Kanda
(ii) Kila sekta kutoka Kanda iwe na mwakilishi mmoja (1)
(iii) Katibu wa Kanda awe Katibu wa Kamati

5.3.2. Wenyeviti wote wa Kamati za wanawake kutoka matawini ndio watakaounda mkutano Mkuu wa Kanda wa wanawake. Mkutano wa Kanda wa wanawake utamchagua.

- Mwenyekiti wa Kamati ya Wanawake Kanda atakuwa mjumbe wa Mkutano Mkuu na Baraza Kuu TPAWU Taifa.

- Wajumbe wa Kanda kama ilivyo katika ibara 5.3.2.

5.4. **Kamati ya wanawake ya Taifa**:

5.4.1. (i) Wajumbe wote wanaowakilisha wanawake katika Mkutano Mkuu
(ii) Wajumbe watamchagua Mwenyekiti wao wa Taifa
(iii) Wajumbe wanne (4) wanawake watakaohudhuria mikutano ya Baraza Kuu.
(iv) Katibu wa Kamati ya Wanawake taifa atakuwa ni mtendaji wa chama anayeshughulikia masuala ya wanawake.

**6.0. MAJUKUMU YA KILA NGAZI YA KAMATI ZA WANAWAKE**

**6.1. TAWI**

(i) Kuwahamasisha wafanyakazi wanawake wajiunge na chama cha wafanyakazi
(ii) Kuchambua na kuyajadili mahitaji ya wanfanyakazi wanawake na kuyawasilisha katika vyombo vinavyohusika
(iii) Kuwaunganisha wafanyakazi wanawake kwa njia ya umoja na mshikamano

(iv) Kuweka takwimu na taarifa mabli mbali kuhusu wafanyakazi wanawake.
(v) Kwa kushirikiana na kamati za tawi kuwaelimisha wanachama/ wafanyakazi kuhusu haki zao na wajibu wao kazini
(vi) Kubuni mbinu na utatuzi wa matatizo wafanyakazi wanawake amani na upendo baina ya wafanyakazi wanawake na wanaume.

(vii) Kuitisha mikutano ya kujadili masuala yanayohusu wafanyakazi wanawake.
(viii) Kufanya mawasiliano na chama cha wafanyakazi ngazi inayohusika na kutoa mlisho nyuma kwa wahusika.

**6.2. KANDA:**

(i) Kuhakikisha kuwa kamati za wanawake zipo kwa mujibu wa Katiba ya TPAWU na zinafanya kazi.

(ii) Kupokea, kujadili na kufanyia kazi mapendekezo mbali mbali kutoka matawini.

(iii) Kuhamasisha wafanyakazi wanawake kujiunga na chama hiki itafanywa kwa kushirikiana na Halmashauri ya tawi mahali pa kazi pamoja na kamati ya wanawake.

(iv) Kutoa elimu kwa wafanyakazi wanawake juu ya masuala mbalimbali.

(v) Kufuatilia utekelezaji wa majukumu mbalimbali yanayohusu wanawake na maamuzi mbali mbali yaliyotolewa na ngazi ya Kanda na Taifa katika Matawi.

(vi) Kubuni mbinu mbalimbali ili kuwawezesha wanawake kuongeza kipato na kuboresha maisha na mazingira ya kazi.

(vii) Kushauri chama ngazi ya Kanda juu ya masuala ya maendeleo kwa wanawake.

**6.3. TAIFA:**

(i) Kuhakikisha kuwa Kamati za wanawake zinaundwa na kufanya kazi kwa mujibu wa katiba ya TPAWU.

(ii) Kutoa elimu katika ngazi zote za chama kuhusu masuala ya wanawake katika kuongeza kipato na kuboresha mazingira na makazi.

(iii) Kubuni mbinu mbalimbali ili kuwawezesha wanawake kushiriki uongozi katika ngazi zote, Kuongeza kipato na kuboresha mazingira/makazi.

(iv) Kufanya tathmini ya shughuli za wafanyakazi wanawake angalau mara moja kwa mwaka na kuratibu mapendekezo yanatoka ngazi zote za chama.

(v) Kamati ya wanawake Taifa itakutana kabla ya vikao vya Baraza Kuu.

## 7.0. MUUNDO WA KAMATI YA VIJANA

Kutakuwa na kamati ya vijana ya TPAWU ambacho ni chombo cha ushauri kwa kamati ya utendaji kuhusu masuala ya vijana. ( kijana ni mtu mwenye umri kati ya 18 – 35).

7.1. Muundo wa Kamati za Vijana

7.1.1. Kamati ya Vijana katika tawi

Kamati ya vijana tawini yenye wafanyakazi vijana

(i) 1-100 wajumbe wanne (4) ***jinsia izingatiwe***.
(ii) 101-na kuendelea Wajumbe watano(5) akiewepo Mwenyekiti na Katibu ***(jinsia izingatiwe).***
(iii) Mwenyekiti na Katibu wa Kamati ya Vijana atakuwa mjumbe katika Halmashauri ya tawi.
(iv) Wajumbe wa Kamati hii watachaguliwa kila baada ya miaka mitano.
(v) ***Vikao vya kamati ya vijana tawi vitakutana kabla ya kikao cha Halmashauri ya tawi***.

### 7.1.2. Kamati ya Vijana Kanda

Kamati ya vijana kanda itakuwa na wajumbe watano (5) wenye sifa zifuatazo:-

(i) Watokane na mkutano mkuu wa kanda
(ii) Wajumbe watachagua mwenyekiti na katibu
(iii) Wenyeviti wote wa kamati ya vijana kutoka matawini ndiyo watakaunda mkutano wa kanda wa vijana
(iv) Mwenyekiti wa kamati ya vijana kanda atakuwa mjumbe wa mkutano mkuu na baraza kuu la TPAWU Taifa.
(v) Wajumbe wa kamati hii watachaguliwa kila baada ya miaka mitano.

7.1.3. Kamati ya Vijana ya Taifa

(i) Wajumbe wote wanaowakilisha vijana katika mkutano mkuu.
(ii) Wajumbe watamchagua mwenyekiti wao wa Taifa.
(iii) Wajumbe wa kamati hii watachaguliwa kila baada ya miaka mitano.

## 7.2. MAJUKUMU YA KILA NGAZI YA KAMATI ZA VIJANA

### 7.2.1 TAWI

(i) Kuwahamasisha wafanyakazi vijana wajiunge na chama cha TPAWU.
(ii) Kupigania ongezeko la ajira na mazingira mazuri ya kazi kwa vijana.
(iii) Kuchambua na kuyajadili mahitaji ya wafanyakazi vijana na kuyawasilisha katika vyombo vinavyohusika.
(iv) Kuwaunganisha wafanyakazi vijana kwa njia ya umoja na mshikamano.
(v) Kuweka takwimu na taarifa mbalimbali kuhusu wafanyakazi vijana.
(vi) Kushirikiana na kamati za tawi kuwaelimisha wanachama /wafanyakazi kuhusu haki zao na wajibu wao kazini.
(vii) Kubuni mbinu na utatuzi wa matatizo ya wafanyakazi vijana.
(viii) Kuitisha mikutano ya kujadili masual yanayohusu wafanyakazi vijana.
(ix) Kamati ya vijana tawi itakutana mara moja kwa mwezi.

### 7.2.2. KANDA

i. Kuhakikisha kuwa kamati za vijana ngazi ya tawi zipo kwa mujibu wa katiba ya TPAWU na zinafanya kazi
ii. Kupigania ongezeko la ajira na mazingira mazuri ya kazi kwa vijana.
iii. Kupokea , kujadili na kufanyia kazi mapendekezo mbalimbali kutoka kamati z a vijana ngazi ya tawi
iv. Kuhamasisha wafanyakazi vijana kujiunga na chama kwa kushirikiana na uongozi wa Kanda
v. Kutoa elimu kwa wafanyakazi vijana juu ya masuala mbalimbali kama sheria za kazi.
vi. Kufuatilia utekelezaji wa majukumu mbalimbali yanayohusu vijana na maamuzi mbalimbali yalitolewa na ngazi ya kanda na Taifa katika matawi.
vii. Kushauri chama ngazi ya Kanda juu ya masuala ya maendeleo kwa vijana.
viii. Kamati ya Vijana Kanda itakutana mara baada ya vikao vya kamati ya wanawake kanda na kabla ya Kamati ya Utendaji Kanda.

7.2.3. **TAIFA**

i. Kuhakikisha kuwa kamati za vijana ngazi ya Kanda zipo kwa mujibu wa katiba ya TPAWU na zinafanya kazi.
ii. Kupigania ongezeko la ajira na mazingira mazuri a kazi kwa vijana.
iii. Kupokea, kujadili na kufanyia kazi mapendekezo mbalimbali kutoka kamati za vijana ngazi ya kanda.
iv. Kuhamasisha wafanyakazi vijana wanajiunga na chama kwa kushirikiana na uongozi mwingine.

v. Kutoa elimu kwa wafanyakazi vijana juu ya masuala mbalimbali.

vi. Kufuatilia utekelezaji wa majukumu mbalimbali yanayohusu vijana na maamuzi mbalimbali yalitolewa na ngazi ya Kanda na Taifa.

vii. Kushauri chama ngazi ya kanda juu ya masuala ya maendeleo kwa vijana.

viii. Kamati ya Vijana ***Taifa*** itakutana mara baada ya vikao vya Kamati ya Wanawake Taifa na kabla ya Kamati ya Utendaji Taifa.

**8.0. MUUNDO WA KANDA ZA TPAWU:**

8.1. (a) Kanda inaweza kufunguliwa katika eneo lolote lenye idadi ya wanachama wanaofikia (2,500) elfu mbili na mia tano.

(b) ***Ikiwa Kanda hiyo itafikisha wanachama zaidi ya (15,000) elfu kumi na tano, Kamati ya Utendaji Taifa inaweza kupendekeza kwa Baraza Kuu kufunguliwa kwa Kanda nyingine ilimradi isiwe kwenye mkoa mmoja***.

(c) ***Endapo Kanda itapungukiwa na wanachama chini ya (2,500) elfu mbili na mia tano, Kanda hiyo itapewa muda wa miezi ishirini na nne (24) kuongeza wanachama na ikishindwa kufikisha kiwango tajwa hapo juu, Kamati ya Utendaji Taifa itapendekeza kwa Baraza Kuu kufutwa kwa Kanda hiyo.***

8.2. Vikao vya Chama vya Kanda:

8.2.1. Kutakuwa na vikao vifuatavyo katika ngazi ya Kanda:

(a) Mkutano Mkuu wa Kanda
(b) Kamati ya Utendaji ya Kanda

**8.2.1.1. Mkutano Mkuu wa Kanda:**

Mkutano Mkuu wa Kanda ndicho chombo kikuu cha chama katika Kanda na utafanya mkutano wake mara moja kila baada ya miaka mitano (5) Hata hivyo kwa uamuzi wa vyombo vya juu vya chama mkutano maalum unaweza kuitishwa. Mkutano Mkuu wa Kanda utakuwa na wajumbe wafuatao:

(a) Mwenyekiti wa Kanda
(b) Katibu wa Kanda- atakuwa Katibu wa Kamati ya utendaji ya Kanda.
(c) Wajumbe waliochaguliwa sawa na 4.8.1.
(d) Makatibu wa sehemu
(e) Makatibu wasaidizi wa Sehemu.
(f) Maafisa wengine wakuteuliwa wanaweza kualikwa kuhudhuria Mkutano Mkuu wa Kanda kwa mujibu wa nyadhifa zao lakini watakuwa hawana haki ya kupiga kura.
(g) Mwenyekiti wa Kamati ya wanawake Kanda.
(h) ***Mwenyekiti wa Kamati ya Vijana Kanda.***

**8.3. Mkutano Mkuu wa Kanda utafanya kazi zifuatazo:**

(a) Kupokea na kushughulikia taarifa zilizoletwa na Kawmati ya Utendaji ya Kanda
(b) Kutekeleza maazimio yaliyotolewa na vyombo vya juu katika chama.
(c) Kuratibu na kusaidia katika utekelezaji wa shughuli za chama katika Kanda.
(d) Kujadili na kukuza hali ya maisha ya wafanyakazi ambao ni wanachama katika Kanda

8.3.1. **Mkutano Mkuu wa Kanda utachagua wanachama wafuatao**:

(a) Mwenyekiti wa Kanda
(b Wajumbe wa Kamati ya Utendaji ya Kanda
(c) Wajumbe watakaoiwakilisha Kanda katika Mkutano Mkuu wa Chama wa Taifa mmoja kwa kila sehemu katika chama.
(d) Mwenyekiti wa Kanda ataendelea kuwa mjumbe mpaka uchaguzi wa kanda utakapomalizika.

8.4. **Kamati ya Utendaji ya Kanda**:

8.4.1. Kutakuwa na Kamati ya Utendaji ya Kanda itakayokutana mara moja ***kwa mwaka.*** Kamati hii itakuwa na wajumbe wafuatao:

(a) Mwenyekiti wa Kanda
(b) Katibu wa Kanda
(c) Wajumbe wawili kwa kila sekta ya chama waliochaguliwa na Mkutano Mkuu wa Kanda.
(d) Wajumbe wa Baraza Kuu walioko katika Kanda hiyo.
(e) Mwenyekiti wa Kamati ya Wanawake Kanda.
***(f) Katibu wa Sehemu***
***(g) Mwenyekiti wa Kamati ya Vijana Kanda***

8.4.2. Kazi za Kamati ya Utendaji ya Kanda:-

8.4.3. Kamati ya Utendaji ya Kanda itafanya kazi zifuatazo:

(a) Kutekeleza maazimio ya vyombo vya juu vya chama.
(b) Kuratibu na kusaidia katika utekelezaji wa shughuli za chama katika Kanda.
(c) Kusaidia matawi katika shughuli mbalimbali za kuimarisha chama.

9.0. **Viongozi wa Kanda na kazi wao**:

9.1. **Mwenyekiti wa Kanda**:

8.2. Mwenyekiti wa Kanda atafanya kazi kama za Mwenyekiti wa Taifa katika Kanda yake.

9.3. Katibu wa Kanda:

9.3.1. Katibu wa Kanda atakuwa ndiye Mtendaji Mkuu wa chama katika Kanda na atafanya kazi chini ya maelekezo ya Katibu Mkuu.

9.3.2. Katibu wa Kanda atafanya kazi zifuatazo kwa mujibu wa Katiba ya Chama:

(a) Atahudhuria mikutano yote ya chama katika Kanda na atakuwa na haki ya kupiga kura.
(b) Atatia sahihi katika hundi zote na atawajibika kufanya mawasiliano yote yanayohusika.
(c) Atatunza vitabu vyote pamoja na mali za chama kama atakavyoamriwa na Katibu Mkuu.

(d) Atakuwa Mtendaji Mkuu wa chama katika Kanda
(e) Atapeleka benki fedha zote alizokusanya kutoka katika matawi yote yaliyo katika Kanda husika
(f) Atawasilisha kila baada ya miezi mitatu taarifa ya kazi, mapato na matumizi kwa Katibu Mkuu.
(g) Atatuma kwa kila mjumbe wa Kamati ya Utendaji ya Kanda wito wa mikutano angalau siku 14 kabla ya mikutano kufanyika.
(h) Atawahamasisha wafanyakazi ili wajiunge na chama kwa k8ushirirkiana na Makatibu walio chini yake.
(i) Atawasilisha kwa Katibu Mkuu taarifa ya fedha na maendeleo ya chama katika Kanda kwa kadri ya maelekezo ya Kamati ya Utendaji ya Taifa/Katibu Mkuu.

## 10.0. CHAMA NGAZI YA TAIFA, SEKTA, IDARA NA KANDA:

10.1. Wasaidizi wa Katibu Mkuu

Chama Makao Makuu kitakuwa na wasaidizi wa Katibu Mkuu watakao shughulikia idara na sekta za chama

10.2. **Idara**:

10.2.1. Kutakuwa na Idara zifuatazo za chama:

(a) Idara ya Elimu, Wanawake na Vijana.
(b) Idara ya Uchumi, Utafiti na Mikopo.
(c) Idara ya Uhasibu na Utumishi.

## 10.3. KANDA NA SEHEMU:

10.3.1. Chama kitakuwa na Kanda nane (8) kwa kuanzia na kupanuka/kupungua kieneo kwa kadri ya uwezo wa chama kifedha na wingi wa wanachama.

### 10.3.2. Kanda za TPAWU zitakuwa zifuatazo:

**1. ARUSHA:**

Mkoa wa Arusha
Mkoa wa Singida
Mkoa wa Manyara

**2.** **IRINGA:**

Mkoa wa Iringa
***Mkoa wa Njombe***

**3.** **MBEYA:**

Mkoa wa Mbeya
Mkoa wa Tabora
Mkoa wa Kigoma
**Mkoa wa Katavi**

**4.** **MOROGORO**

Mkoa wa Morogoro
Mkoa wa Pwani
Mkoa wa Dar es Salaam
Mkoa wa Dodoma

**5.** **KILIMANJARO**

**Mkoa wa Kilimanjaro**

**6.** **MTWARA:**

Mkoa wa Mtwara
Mkoa wa Lindi
Mkoa wa Ruvuma

**7.** **ZIWA:**

Mkoa wa Mwanza
Mkoa wa Kagera
Mkoa wa Mara
Mkoa wa Shinyanga
Mkoa wa Simiyu
Mkoa wa Geita

**8.** **TANGA:**

Mkoa wa Tanga

## 11.0. MKUTANO MKUU WA CHAMA WA TAIFA:

11.1. ***Kabla ya uchaguzi Katibu Mkuu atatangaza nafasi zote za uongozi katika chama kwa wanachama hai na wale watakaopenda kugombea nafasi hizo watajaza fomu na kuzirejesha ofisi ya Katibu Kuu ndani ya kipindi kitakachoainishwa katika tangazo***.

11.2. Mkutano Mkuu wa Chama utahudhuriwa na wajumbe walichaguliwa kutoka kila Kanda ya Chama. MMoja kutoka kila sekta ya Chama katika Kanda. Zaidi ya wajumbe hao, mkutano Mkuu wa chama utahudhuriwa na hawa wafuatao:

(i) Mwenyekiti wa Chama wa Taifa
(ii) Katibu Mkuu wa Chama
(iii) Naibu Katibu Mkuu
(iv) Wasaidizi wa Katibu Mkuu
(v) Wakuu wa Idara za chama
(vi) Wenyeviti wa Kanda
(vii) Mjumbe mwanamke kutoka kila Kanda
(viii) Wadhamini ***wa chama***
(ix) Makatibu wa Kanda
(x) Makatibu wa Sehemu
(xi) Makatibu wasaidizi wa Sehemu zinazojitegemea
(xii) Wenyeviti Kamati za wanawake Kanda
(xiii) ***Wenyeviti wa Kamati za Vijana Kanda***

11.3. Mwenyekiti wa Taifa wa TPAWU na Katibu Mkuu wataendelea na kuwa wajumbe wa Mkutano Mkuu na Baraza Kuu mpka uchaguzi utakapomalizika na watakuwa na haki ya kugombea/ kuchaguliwa.

11.4. Mkutano Mkuu wa ***uchaguzi*** wa Chama ***utafanyika kila baada ya miaka mitano (5) na Mkutano Mkuu wa kazi utafanyika kila baada ya miaka miwili na nusu (2½) baada ya Mkutano Mkuu wa uchaguzi***.

11.5. Kama kutatokea sababu maalum, Kamati ya Utendaji ya chama au theluthi mbili ya wajumbe wa Baraza Kuu wanaweza kuamua kuitisha kikao cha Mkutano Mkuu maalum. Mkutano Mkuu maalumu utajadili mambo yale tu yaliyosababisha kuitishwa kwake.

11.6. Taarifa ya Mkutano Mkuu wa chama itatolewa angalu miezi mitatu kabla. Taarifa ya muda mfupi inaweza kutolewa kama itabidi kuitisha Mkutano Mkuu maalum.

11.7. Kiwango cha chini cha mahudhurio ya Mkutano Mkuu wa chama kitakuwa ni theluthi mbili ya wajumbe wote.

11.8. Mwenyekiti wa Mkutano Mkuu atakuwa ni yule Mwenyekiti wa Chama wa Taifa. Iwapo kwa sababu zozote zile Mwenyekiti atashindwa kuhudhuria mkutano mkuu utachagua Mwenyekiti wa mkutano huo miongoni mwa wajumbe waliohudhuria.

11.9. Kazi za Mkutano Mkuu wa Chama:-

11.9.1. Mkutano Mkuu wa chama ndicho chombo kikuu cha chama kitakachokuwa na mamlaka ya juu kuliko vikao vingine.

11.9.2. Mkutano Mkuu wa chama utachagua wafuataao:

(a) Mwenyekit wa Chama wa Taifa
(b) Katibu Mkuu
(c) Wajumbe wa Baraza Kuu mmoja kutoka kila Kanda na wajumbe wa chama katika Mkutano Mkuu Shirikisho.
(d) Wawakilishi wa TPAWU katika Mkutano Mkuu wa Shirikisho. Watakuwa wajumbe ***thelathini (30)*** wakiwemo:
    (1) Mwenyekiti wa TPAWU Taifa
    (2) Katibu Mkuu
    (3) Mwenyekiti wa Kamati ya Wanawake Taifa
    (4) Mjumbe mmoja wa Kamati ya Utendaji ya Shirikisho.
    (5) Wajumbe watatu (***8)*** mmoja mwanamke wa kuchaguliwa na Baraza Kuu kuingia Baraza Kuu la shirikisho
    (6) Wajumbe ***16*** wa kuchaguliwa na Mkutano Mkuu
    (7) Mjumbe mmoja mwakilishi wa wanawake kwenye mkutano wa Shirikisho.
    (8) ***Mwenyekiti wa Kamati ya Vijana Taifa***

TPAWU itafuata katiba ya Shirikisho kupata idadi sahihi ya wajumbe wa vikao vya shirikisho mara kwa mara.

11.9.3. Mkutano Mkuu wa chama ndiyo chombo pekee kitakachokuwa na mamlaka ya krekebisha au kufanyia mabadiliko katiba ya chama. Mkutano Mkuu wa chama utapokea na kurekebisha katiba ya chama bila kuathiri sheria.

11.9.4. Mkutano Mkuu wa chama utajadili na kutoa uamuzi kuhusu taarifa za kazi a fedha zilizoletwa na Kamati Kuu ya Utendaji ya Chama.

11.9.5. Mkutano Mkuu wa chama utakuwa na uwezo wa kuthibitisha,kurekebisha au kufuta uamuzi wowote uliopitishwa na kikao au kiongozi yeyote wa chama.

11.9.6. Mkutano Mkuu ndio utakaotoa uamuzi kuhusu ghughuli za uhusiano wa Kimataifa na kuhusu chama kujiunga na Taasisi za vyama vya Kimataifa.

11.9.7. Mkutano Mkuu wa chama utafanya kikao chake mara moja kila baada ya miaka mitano (5) na unaweza kukasimu madaraka yake kwa Baraza Kuu.

**11.9.8. Haki ya kuchaguliwa:-**

Kila mwanachama asiyelaza michango yake katika chama atakuwa na haki ya kuchaguliwa kuwa mjumbe wa Mkutano Mkuu wa chama isipokuwa wanachama wa heshima.

**11.9.9. Haki ya Wadhamini:**

Wadhamini wasiochaguliwa na Mkutano Mkuu watakuwa na haki ya kuhudhuria mikutano, kutoa maoni na mapendekezo lakini hawatakuwa na haki ya kupiga kura.

11.9.10. Agenda, Hoja na Mapendekezo:

11.9.10.1. Kamati ya Utendaji ya chama itapendekeza Agenda kwa ajili ya Mkutano Mkuu.

11.9.10.2. Mwanachama au tawi watakuwa na haki ya kupeleka hoja zao katika Mkutano Mkuu wa chama miezi mitatu kabla ya Mkutano Mkuu. Hoja za wanachama hata kama Mkutano Mkuu wa tawi hauziafiki, utaziwasilisha Makao Makuu ya chama kupitia kwa Katibu wa Kanda ili zikajadiliwe na kufanyiwa uamuzi na kamati ya utendaji Taifa.

11.9.10.3. Hoja na mapendekezo vitagawiwa kwa wajumbe wa Mkutano Mkuu kwa maandishi katika muda unaofaa kabla ya mkutano huo.

11.9.11. Utaratibu wa kupiga kura:

11.9.11.1. Uchaguzi utafanyika kwa kura ya siri, uchaguzi wa ***Mwenyekiti wa Taifa, Katibu Mkuu na Naibu Katibu Mkuu utahitaji zaidi ya nusu ya kura zote zilizopigwa ili kutangazwa kuwa wamechaguliwa***.

11.9.11.2. Maamuzi mengine yoyote ya Mkutano Mkuu yatapitishwa kwa nusu ya wajumbe waliopiga kura kwa kuinua mikono, isipokuwa kama Mkutano Mkuu utaamua vinginevyo. Kama kura zitalingana za wagombea, Mwenyekiti wa Mkutano Mkuu atatumia kura yake ya turufu.

11.9.11.3. Mabadiliko yoyote katika katiba/ Kanuni za chama yatapitishwa kwa theluthi mbili ya wajumbe.

## 12.0. BARAZA KUU LA CHAMA LA TAIFA:

12.1.1. Baraza Kuu la Chama litakuwa na wajumbe waliochaguliwakutokana na wajumbe wa Mkutano Mkuu hivyo kwamba kila sekta itawakilishwa na wajumbe atatu. Kikao cha Baraza Kuu la chama kitahudhuriwa vile vile na wajumbe wafutao:

1. Wajumbe wa Kamati ya Utendaji ambao ni:-
   - Mwenyekiti wa TPAWU Taifa
   - Katibu Mkuu
   - Naibu Katibu Mkuu
   - Wenyeviti wa Kanda
   - Wajumbe watatu (3) kutokana na Kapu watachaguliwa iwapo kila sekta ya chama itakuwa imewakilishwa jinsia izingatiwe.
   - Mwenyekiti wa Kamati ya Wanawake Taifa
   - Mjumbe wa Kamati ya Utendaji ya Shirikisho.
   - Wasaidizi wa Katibu Mkuu na Wakuu wa Idara.
   - ***Mwenyekiti wa Kamati ya Vijana Taifa.***

2. Makatibu wa Kanda
3. Wajumbe wanne(4) wanawake
4. Wadhamini wa chama
5. Wenyeviti wa Kamati za wanawake Kanda.

12.1.2. Baraza Kuu la Taifa litakutana mara moja kwa mwaka.

12.1.3. Kamati ya Utendaji inaweza kuitisha kikao maalumu cha Baraza Kuu la Taifa. Kikao cha namna hiyo kinaweza kuitishwa vile vile kama theluthi moja ya wajumbe wa Baraza Kuu la chama wametaka hivyo kwa maandishi.

12.1.4. Taarifa na tarehe ya Mkutano itatolewa mwezi mmoja kabla. Taarifa fupi inaweza ikatolewa kwa ajili ya kikao maalumu cha Baraza Kuu la chama.

12.1.5. Mwenyekiti wa Chama atakuwa Mwenyekiti wa Baraza Kuu la chama la Taifa. Kama kwa sababu zozote zile Mwenyekiti hakuhudhuria mkutano, Baraza Kuu la Taifa litachagua Mwenyekiti wa mkutano huo miongoni mwa wajumbe wake.

**12.2. Kazi za Baraza Kuu la Chama la Taifa:**

12.2.1. Baraza Kuu la Chama litafanya kazi zifuatazo:

(a) Kutayarisha mipango na sera za shughuli za chama kama zilivyotayarishwa na Kamati ya Utendaji ya chama.

(b) Kuhakikisha kwamba shughuli za Kamati ya utendaji na Sekretarieti zinaendeshwa kwa mujibu wa kanuni za vyama vya wafanyakazi.

(c) Kupitisha bajeti ya chama.

(d) Kusikiliza rufaa.

(e) Baraza Kuu la chama litachagua Naibu Katibu Mkuu kutokana na majina yatakayopendekezwa na Kamati ya Utendaji miongoni mwa ***wanachama hai waliojaza fomu ya kuomba nafasi hiyo***. Naibu Katibu Mkuu aliyekuwepo madarakani ataendelea kuwa mjumbe wa Mkutano Mkuu na Baraza Kuu mpaka uchaguzi utakapomalizika.

(f) Litapokea na kujadili taarifa ya kazi za kamati ya wanawake.

(g) Litaamua juu ya uanzishwaji wa Kanda mpya au kufuta Kanda ***baada ya kupokea ya kupokea mapendekezo kutoka Kamati ya Utendaji Taifa***.

(h) Litathibitisha kuchaguliwa kwa Mwenyekiti wa Kamati ya wanawake Taifa.

(i) Litachagua mjumbe/wajumbe wa Kamati ya utendaji ya Taifa "Shirikisho"

(j) ***Litathibitisha kuchaguliwa kwa Mwenyekiti wa Kamati ya Vijana Taifa***.

12.3. **Haki ya kushiriki katika Uchaguzi**:

12.3.1. Kila mwanachama anayelipa michango ya kila mwezi atakuwa na haki ya kuchaguliwa kuwa Mjumbe wa Baraza Kuu la Chama isipokuwa wafuatao:

(a) Maafisa wa chama walikwisha kuchaguliwa na Mkutano Muu.
(b) Wajumbe wa Kamati ya Utendaji ya Chama ***na Wenyeviti wa Kanda***.
(c) Watumishi wengine wa chama
(d) Wanachama wa Heshima

**13.0. KAMATI YA UTENDAJI YA CHAMA:**

13.1. **Muundo wa Kamati**:

13.1.1. Kamati ya Utendaji itakuwa na Mwenyekiti wa chama Taifa. Katibu Mkuu, Naibu Katibu Mkuu, Mwenyekiti wa Kamati ya Wanawake Taifa, ***Mwenyekiti wa Kamati ya Vijana Taifa***, Wenyeviti wa Kanda, wajumbe 3 kutokana na kapu watachaguliwa iwapo kila sekta ya chama itakuwa imewakilishwa na mjumbe wa Kamati ya Utendaji Shirikisho (TUCTA) (jinsia itazingatiwa).

13.2. Kazi za Kamati ya Utendaji ya chama.

13.2.1. Kamati ya Utendaji itawajibika kuhakikisha kwamba mwenendo wote wa shughuli za kazi za chama unafuata kanuni za chama na maazimio ya Baraza Kuu. Kipindi chote kabla ya Baraza Kuu, Kamati ya utendaji itakuwa ndicho chombo cha juu cha kutoa uamuzi, kasoro katika mambo yale ambayo yanalihusu Baraza Kuu la Taifa.

13.2.2. Kupendekeza majina ya wagombea nafasi ya Unaibu Katibu Mkuu kutoka miongoni mwa ***wanachama hai waliojaza fomu za kuomba nafasi hiyo***.

13.2.3. Kamati ya Utendaji itathibitisha mapendekezo ya ajira yatakayoletwa kwake na Ofisi ya Katibu Mkuu kwa kuzingatiwa kanuni za utumishi za chama.

13.2.4. ***Kuandaa kanuni za katiba ya chama.***

13.3. **Nafasi zilizowazi:**

**13.3.1. Mjumbe wa Kamati ya Utendaji au Baraza Kuu la taifa ataacha kuwa mjumbe na nafasi yake itatangazwa kuwa iko wazi baada ya haya yafuatayo kutokea:-**

(i) Akihama chama
(ii) Akifukuzwa katika chama
(iii) Akisimamishwa na Baraza Kuu la Taifa
(iv) Akikosa kuhudhuria vikao viwili mfululizo vya Kamati ya Utendaji au Baraza Kuu la Taifa bila sababu za kuridhisha
(v) Akiacha kazi au kufariki.
(vi) Akipata uhamisho wa kudumu nje ya sehemu au Kanda aliyochaguliwa, atakapopatikana na hatia ya shitaka la kesi ya jinai, ugonjwa au kusimamishwa kazi kwa zaidi ya miezi 6.

**13.4. Mikutano**:

13.4.1. Kamati ya Utendaji itakutana sio chini ya mara mbili kwa mwaka.

13.5. **Viongozi wa Kitaifa:**

**13.5.1. Uchaguzi:**

Uchaguzi wa Mwenyekiti wa Taifa, Katibu Mkuu, ***wajumbe wa Baraza Kuu la TPAWU, wajumbe wa Baraza Kuu la TUCTA na wajumbe wa Mkutano Mkuu wa TUCTA kama ilivyoainishwa katika kifungu*** 10.9.2. cha katiba ya chama.

**13.5.2. Uteuzi:**

Maafisa wengine watateuliwa na Kamati ya Utendaji ya Taifa.

**13.6. Mwenyekiti wa Taifa:**

**Mwenyekiti wa Taifa atatokana na wajumbe wa Mkutano Mkuu wa Taifa na atafaya kazi zifuatazo:**

(a) Atahudhuria Mkutano Mkuu, Baraza Kuu na Kamati ya Utendaji Taifa.

(b) Atasimamia na kuongoza Mkutano Mkuu, Baraza Kuu na Kamati ya Utendaji na mikutano mingine ambayo Kamati ya Utendaji ya chama itaamua.
(c) Atawajibika katika usimamizi wa nidhamu katika Mikutano.
(d) Atatia sahihi kumbukumbu za mikutano pamoja na Katibu Mkuu wa Taifa.
(e) Atahakikisha kuwa katiba na taratibu za chama zinafuatwa na wale wote wanaohusika.
(f) Katika mikutano inayoongozwa na Mwenyekiti wa Taifa atakuwa na kura ya turufu, kinga licha ya kura yake ya kawaida.
(g) Ikiwa Mwenyekiti wa Taifa atakuwa na udhuru wa kumfanya asiweze kuhudhuria mkutano, mjumbe yeyote atakayechaguliwa na mkutano huo atendesha shughuli za mkutano.
(h) Ikiwa kiti cha Mwenyekiti kitabaki wazi kwa sababu yoyote ile kabla ya Mkutano Mkuu wa chama Katibu Mkuu atatoa taarifa kwa Kamati ya Utendaji Taifa na nafasi hiyo itajazwa na Baraza Kuu la Taifa mpaka Mkutano Mkuu mwingine utakapofanyika

**13.7. Katibu Mkuu wa Chama**

Katibu Mkuu atachaguliwa kila baada ya miaka mitano na atakuwa ndiye mtendaji Mkuu na msemaji Mkuu wa chama atakayewajibika katika utekelezaji wa maamuzi yaliyokwisha kupitishwa na Mkutano Mkuu, Baraza Kuu na Kamati ya Utendaji ya chama. ***Katibu Mkuu atachaguliwa na Mkutano Mkuu kutoka miongoni mwa wanachama hai waliojaza fomu kwa nafasi hiyo*** na atafanya kazi zifuatazo:-

(a) Atahudhuria Mkutano Mkuu, Baraza Kuu na Kamati ya Utendaji Taifa.

(b) Ataweka kumbukumbu za mikutano na kutekeleza sera za chama pamoja na maamuzi yaliyokwisha kupitishwa na Mkutano Mkuu, Baraza Kuu na Kamati ya Utendaji Taifa.

(c) Atatayarisha na kuwasilisha mbele ya Kamati Kuu ya Utendaji ya Taifa, siyo chini ya robo mwaka, na kila mwisho wa mwaka wa fedha, hesabu sahihi ya mapato na matumizi ya chama pamoja na kuwasaidia wakaguzi wa hesabu za fedha za chama atakapotakiwa kufanya hivyo.

(d) Atawajibika kwa chama kuhusu fedha zote zinazopitia mikononi mwake.

(e) Atawajibika kutunza vitabu vya fedha na vitabu vingine vya mahesabu ya fedha Makao Makuu, kutuza fedha ya matumizi ya kila sikum kufanya malipo kwa niaba ya chama na kutunza nakala zote za stakabadhi za mapato na matumizi

(f) Atatoa stakabadhi kwa fedha yote iliyopokelewa na chama

(g) Atatayarisha hundi zote na hali za malipo, ambazo zitasainiwa na angalu mdhamini mmoja na Katibu Mkuu au Msaidizi wake.

(h) Atatuma kwa kila mjumbe wa Kamati ya Utendaji ya Taifa agenda za mikutano angalu siku 14 kabla ya mikutano hiyo.

(i) Kwa mujibu wa katiba hii Katibu Mkuu anaweza kuongeza muda wa uongozi/kiongozi wa tawi pale anaporidhika kwamba kuna sababu za msingi za kufanya hivyo.

**13.8. Naibu Katibu Mkuu:**

Naibu Katibu Mkuu atawajibika kwa kufanya kazi atakazoagizwa na Katibu Mkuu, Katibu Mkuu anapokuwa hayupo atafanya kazi zote za Katibu Mkuu.

**14.0. BARAZA LA WADHAMINI WA CHAMA:**

**14.1. Wadhamini wa chama:**

14.1.1. Kutakuwa na Wadhamini watatu walioteuliwa na Mwenyekiti wa Taifa wa TPAWU kwa kushauriana na Katibu Mkuu wa chama na kuthibitishwa na Baraza kuu.

- (a) Wawe na uzoefu wa kutosha katika masuala ya vyama vya wafanyakazi.
- (b) Wasiwe na madaraka ya kudumu katika chama
- (c) Wawe wanaishi katika eneo ambalo siyo mbali sana na mji ambao Makao Makuu ya chama yapo.
- (d) Wawe bado ni wafanyakazi walioajiriwa.

14.1.2. Fedha na mali za chama vitawekwa katika rasilimali chaini ya udhamini wa Baraza la wadhamini ambao watatunza rasilimali hii kwa kadri Kamati ya Utendaji itakavyoelekeza.

14.1.3. Nafasi ya mdhamini wa chama itatangazwa kuwa iko wazi na Kamati ya utendaji Taifa. Mdhamini atahesabika kuwa ameondolewa katika shughuli zake iwapo mambo yafuatayo yatatokea:-

(a) Atafariki
(b) Atajiuzulu
(c) Atakuwa na akili zisizo timamu
(d) Atapatikana na hatia ya shitaka la jinai au asipotekeleza kazi za udhamini kwa muda unaozidi miezi sita .
(e) Akiacha kazi

14.1.4. Mdhamini anaweza kujiuzulu wakati wowote kwa kumwandikia barua Katibu Mkuu wa Chama.

14.1.5. Kila maazimio yatakayoteua wadhamini yataingizwa katika kumbukumbu za kikao kilichowathibitisha.

14.1.6. Hati zote za kumiliki mali inayoondosheka na isiyoondosheka na hati nyingine zozote za chama zitakuwa tayari kutazamwa na wadhamini kila watakapotaka kufanya hivyo. Ili mradi tu ifahamike kwamba hati zote zinazohisiana na milki ya mali zitakuwa zinatunzwa na Katibu Kuu ambaye atazitoa kwa wadhamini kila watakapozihitaji. Kila anapokabidhi kwa wadhamini Katibu Mkuu atatoa hati ya makabidhinao ambayo itaelezea vile vile ni lini hati hizo zinaweza kuhitajika na chama kwa shughuli za kila siku ili utendaji usiathiriwe na kutokuwepo kwa hati hizo.

14.1.7. Mdhamini aliyejiuzulu au kuondolewa katika nafasi hiyo kwa sababu zozote atawajibika kukabidhi hati na mali zote za chama alizomiliki kwa wadhamini wengine.

14.1.8. Suala la uwekezji rasilimali litaamriwa na Kamati ya Utendaji Taifa. Mdhamini haruhusiwi kutumia/kuwekkeza mali yoyote ya chama kwa faida yake.

14.1.9. Mwanachama asiyelipa michango ya kila mwezi hawezi kuchaguliwa kuwa mdhamini, na yule abaye ni mdhamini atajiuzulu kazi hiyo mara baada ya kuacha kuwa mfanyakazi.

**15.0. MENGINEYO:**

15.1. Kiwango cha mahudhurio ya mikutano:

15.1.1. Bila kuathiri yaliyomo katika baadhi ya vifungu vya kanuni hizi, kiwango cha mahudhurio kwa mikutano yote ya chama itakuwa ni zaidi ya nusu ya wajumbe wanaotakiwa kuhudhuria mkutano huo.

15.1.2. Kujaza nafasi zilizowazi:

Kila nafasi itakapoachwa wazi katika chama, kikao kinachohusika kitaijaza mapema iwezekanavyo kwa mujibu wa Katiba hii.

**Ngazi ya Kanda:** Kamati ya Utendaji itachagua mtu kuziba nafasi iliyo wazi katika Kanda hiyo hadi kitakapofanyika kikao husika cha kikatiba.Ngazi ya Taifa: Kamati ya Utendaji ya Taifa itachagua mtu wa kuziba nafasi iliyo wazi hadi kitakapofanyka kikao husika cha kikatiba.

**15.1.3. Kujiuzulu:**

15.1.3.1. Mwanachama anayetaka kujiuzulu anaweza kufanya hivyo kwa kuwasilisha barua yake kwa Katibu wa Tawi wa chama.

15.1.3.2. Kiongozi wa chama anayetaka kujiuzulu anaweza kufanya hivyo kwa kuandika barua kwa Katibu wa chombo kilichomchagua au kma aliteuliwa kwa kupeleka barua hiyo kwa mamlaka iliyomteua

15.1.4. Kujitolea kwa ajili ya chama:
Viongozi na Maafisa wote wa chama watajitolea kukitumikia chama na hawatajiingiza katika madaraka ya kisiasa nje ya chama bila ridhaa ya kikao kilichomchagua. Nafasi hiyo iwe ya kuchaguliwa au ya kuajiriwa

**15.1.5. Kusimamishwa/Kufukuzwa uongozi:**

15.1.5.1. Kiongozi yeyote wa kuchaguliwa katika ngazi ya tawi ambaye ni: Mjumbe wa tawi, Halmashauri ya tawi, Katibu wa tawi, Mwenyekiti wa tawi, Mjumbe Kamati ya wanawake, Mwenyekiti kamati ya wanawake, Katibu kamati ya wanawake, ***Mwenyekiti wa Kamati ya Vijana na Katibu wa Kamati ya Viajana*** atakayekwenda kinyume cha katiba ya TPAWU au kufanya vitendo

vya kukisaliti chama atasimamishwa uongozi/uanachama na Katibu wa Kanda. Katibu wa Kanda katika kipindi kisichozidi miezi sita (6) ataitisha Kamati ya Utendaji Kanda ili kujadili suala la kiongozi/viongozi waliosimamishwa uanachama/uongozi. Kamati ya utendaji Kanda inapewa mamlaka ya kuwaonya/kuwafukuza viongozi wa chama ikiwa itathibitika kwamba wamefanya vitendo vya kukisaliti chama na kuhatarisha mwenendo mzima wa chama.

15.1.5.2. Viongozi waliochaguliwa na Mkutano Mkuu watasiamishwa uongozi na Baraza Kuu la Taifa, lakini watakuwa na haki ya kuomba rufaakwenye Mkutano Mkuu wa Taifa. Bila kuathiri maelezo hayo, uamuzi wa kusimamishwa na Baraza Kuu utakuwa na nguvu na utaanza kazi mara moja mpaka Mkutano Mkuu utakapoamua vinginevyo.

15.1.5.3. Kiongozi aliyechaguliwa na mkutano mkutano wa Kanda, Baraza kuu au Kamati ya Utendaji atasimamishwa uongozi na Katibu Mkuu. Na katika kipindi kisichozidi miezi sita (6) Katibu7 Mkuu ataitisha kamati ya utendaji ili kutoa maamuzi kuhusu suala hilo.

15.1.5.4. Kiongozi yeyote atakeyesimamishwa uongozi anaweza kuomba rufaa katika kikao cha juu ya kile kilichomsimamisha/Kumfukuza.

**15.2. Mahudhurio ya Mikutano:**

Mjumbe wa mamlaka yoyote katika chama ayeliewekwa kwa mujibu wa kanuni hizi atacha kuwa mjumbe kama atshindwa kuhudhuria mikutano miwili mfululizo bila sababu za kuridhish kwa mamlaka inayohusika.

**15.3. Mapato ya chama:**

15.3.1. Chama kitaendesha shughuli zake kutokana na fedha iliyotokana na kiingilio, michango ya kila mwezi, misaada kutoka kwa wafadhili/Wahisani, Miradi ya uchumi ya chama, misaada kutoka kwa vyama rafiki, na michango maalumu ya wanachama.

15.3.2. Mhasibu Mkuu atakuwa na wajibu na majukumu ya utunzaji wa kumbukumbu zote za fedha za chama na atawajibika kutoa taarifa kwa Katibu Mkuu juu ya mapato na matumizi ya fedha za chama kila atakapotakiwa kufanya hivyo kwa mujibu wa kanuni za fedha za chama.

15.4. Hesabu za fedha za chama zitakaguliwa angalau mara moja kwa mwaka na Mkaguzi anayekubalika au Mkaguzi Mahsusi aliyeteuliwa na Kamati ya Utendaji na kuthibitishwa na Baraza Kuu.

15.5. **USULUHISHI**:

Mgogoro wowote utakaotokana na tofauti ya tafsiri ya katiba hii kati ya chama, matawi, kamati zilizochaguliwa, Maafiswa walichaguliwa au wanachama unaweza kupelekwa katika Kamati ya Utendaji ya TUCTA kwa usuluhishi/upatanishi.

**15.6. KUVUNJIKA KWA CHAMA AU KUUNGANISHA VYAMA:**

15.6.1. Kuvunjika chama:

Chama kinaweza kuacha kufanya shughuli zake na kuvunjwa kama pendekezo litapitishwa na theluthi mbili ya wanachama wote. Baada ya chama kulipa madeni yote ikiwa ni pamoja na mafao ya watumishi wa chama mali itakayobaki itakuwa chini ya TUCTA.

15.6.2. Kuunganisha Vyama:

Chama kinaweza kuamua kujivunja baada ya uamuzi wa kutaka kuungana na chama kingine. Uamuzi wa kujiunga na chama kingine unaweza kuchukuliwa na Mkutano Mkuu wa chama ukizingatia maoni yaliyowasilishwa kwa njia ya Hoja, au mapendekezo ya kamati ya utendaji au Baraza Kuu la chama. Hoja hizo na ua mapendekezo yanaweza kupigiwa kura na Mkutano Mkuu, kama wajumbe wake watakuwa wamepata taarifa mwezi mmoja kabla ya mkutano.

15.6.3. Iwapo chama kitavunjwa na kujiunga na chama kingine mali na madeni ya chama hicho yatachukuliwa na chama kipya.

**16.0. MIGOGORO YA KIKAZI: MIJADALA NA MWENENDO:**

**16.1. Sera ya Ujumla:**

(a) Kamati ya utendaji Taifa ya chama itawajibika kwa maazimio yanayotokana na majadiliano na migogoro lakini itakasimu baadhi ya madaraka yake kwa Katibu Mkuu.

(b) Kwa upande wa majadiliano/Mkataba unaohusu sekta nzima ya kikazi itafaa iwapo matawi yenye watu wengi yatahusishwa. Katika hali hiyo, kazi ya Baraza hili itakuwa kutoa ushauri zaidi kwa kuwa ni kamati ya utendaji Taifa na sio Baraza la majadiliano, ambayo itawajibika kwa masuala ya chama.

(c) Baraza la majadiliano linaweza kuchagua mjumbe wa kushughulikia majadiliano na chama cha Waajiri (au mamlaka ya umma yoyote husika). Baraza hili kila mara lazima liongozwe na Katibu Mkuu au mmoja wa Wasaidizi wa sekta inayohusika.

(d) Matawi yana haki ya kujitetea dhidi ya Muajiri na kuendesha shughuli za majadiliano tawini. Hata hivyo, kwa madhumuni ya kuhakikisha kuwa kamati ya utendaji ina mipango mizuri kuhusu sera za mishahara, mikataba ya kwenye matawi itawasilishwa mbele ya Katibu Mkuu kwa uthibitisho kabla ya kutiliana sahihi.

(e) Ili kuzuia migogoro isiyokuwa ya lazima kutokea ni vema kura ya maoni kuhusu mgomo ipigwe katika kikao cha wanachama wote wa Tawi. Maoni yatakayotolewa yatasaidia kutia msukumo kwa Mwajiri:
Hasa kama wengi walipendelea kufanya mgomo. Hali hii inaweza kumfanya Muajiri akapata mawazo ya kukubaliana kufikia kwenye usuluhishi. Ili kuhakikisha kuwa mgomo unaotazamiwa unaungwa mkono na wengi, inafaa ielezwe kwamba maoni sharti yakubaliwe na theluthi mbili ili yawe na nguvu.

(f) Maoni ya kura ya siri ya mgomo yawe tu ni kwa ajili ya kusaidia katika ushauri. Hii ni sawa na kusema kwamba uamuzi wa kugoma lazima uwe ni uamuzi wa kuiomba kamati ya utendaji ya TPAWU kwa ruhusa ya kugoma kwa mgomo wa Kitaifa rejea 15.1(j).

(g) Mgomo mkubwa utahitaji kuratibiwa (bila kufanya hivyo unaweza kuleta hata madhara kwa vyama vingine). Kwa sababu hiyo basi Katiba ya TUCTA itakuwa na aya inayoelezea kuwa kamati ya utendaji ya chama/ vyama itawasilisha kwa Kamati ya Utendaji ya TUCTA maazimio yake ya kuanzisha migomo, hasa ikiwa uamuzi unaweza kuwahusu kiwango kikubwa cha wanachama na chama hicho.

(h) Kwa mgogoro/mgomo kufanikiwa tangu katika mipango mpaka utekelezaji wake, na ili kukwepa adhabu inayoweza kutokana na kuvunja sheria lazima mambo haya yawe na nidhamu yake. Hii ina maana kuwa, hatua za

kinidhamu zitachukuliwa dhidi ya wanaokosa kushiriki mgomo au Halmashauri za matawi zisizoheshimu maazimio ya juu.

(i) Kwa mgogoro/mgomo kufanikiwa inaweza kuwa muhimu na kuamua kufanya utaratibu kuunga mkono wenzetu. Kwa sababu hiyo ndio maana kanuni zinamtaka mwanachama kuheshimu uamuzi uliofanywa na Kamati ya Utendaji Taifa. Hata hivyo, mara nyingi ni vigumu kuwashawishi wanachama kushiriki katika katika kuwaunga mkono wanaogoma hasa kama chama hakiwezi kufidia hasara watakayoipata. Kwa hiyo basi ili kuweza kupata mapato ya kutosha itakuwa ni jambo la maana kwa kamati ya Utendaji Taifa kuanzisha mchango maalumu ambao utachangiwa na wanachama wasioumia sana kutokana na mgomo. (3:7).

Mchango maalumu unapaswa kutumika vile vile kwa kutunzia wanachama walioathiriwa na mgomo wa muda.

(j) Iwapo kamati ya utendaji ya TPAWU itakuwa ndio imetoa uamuzi wa mgomo inapaswa vile vile kuwa tayari kuuliza vyama shiriki vya TUCTA kuanzisha mfuko maalumu wa mgomo.

(k) Utekelezaji mzuri wa kanuni za chama kuhusiana na migogoro/migomo utairahisishia TUCTA kuwa na uwezo wa kuishawishi Serikali kuacha kutunga sheria zisizokubaliana na maslahi ya wafanyakazi.

(l) Kifungu chochote katika Katiba hii kinaweza kubadilika kulingana na matakwa ya sheria za kazi.

(m) Katiba hii haikusudii kuvunja sheria yoyote iliyopitishwa na Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Endapo itatokea kifungu chochote cha Katiba hii Kupingana na sheria za Nchi, Sheria za nchi zitafuatwa.